Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 - 9289]



Issue no: 01 | **Vol no:** 07 | **November** 2026: 188-197

Taswira ya Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu wa Karne ya 21: Uchambuzi wa Shairi la Mahavule na Jamii

Sumaiya Yunus Mwamzandi [(1)]
Mosol Kandagor [(2)]
Magdaline Wafula [(3)]

(1.2.3) Moi University, Kenya.
Main author's email: sumaiyayunus2@gmail.com

Article History
Received: **2026.09.05**
Accepted: **2026.10.10**
Published: **2026.1117**

Cite this article in APA
Mwamzandi, S. Y., Kandagor, M., & Wafula, M. (2026). Taswira ya mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu wa karne ya 21: Uchambuzi wa shairi la Mahavule na Jamii. *Editon consortium journal of Kiswahili, 7(*1), 188-197. https://doi.org/10.51317/jbv7vn05

Ikisiri
Makala haya yanachunguza taswira ya mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu wa karne ya ishirini na moja kwa kurejelea shairi la *Mahavule na Jamii* lililoandikwa na Mahmoud Ahmed Abdulkadir. Madhumuni ya makala haya ni kubaini taswira mbalimbali za mwanamke katika miktadha ya kidini, kifamilia, kijamii na kiteknolojia, pamoja na namna usawiri huo unavyodhihirisha mwingiliano kati ya misingi ya Kiisilamu na mabadiliko ya jamii ya kisasa. Utafiti huu ulifanyika nyanjani na ulichukua muundo wa kimaelezo. Mtafiti alitumia usampulishaji wa kimakusudi kupata mtunzi na mashairi ya Kiswahili ya Kiisilamu. Kupitia mbinu ya mahojiano, mtafiti aliweza kupata idadi ya mashairi matano, *Mahavule na Jamii* likiwa mojawapo. Uchambuzi umeongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Kiisilamu na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo yalibainisha kuwa taswira ya mwanamke katika mashairi ya Kiswahili ya Kiisilamu inaendelea kuwa changamano huku mvutano kati ya mafundisho ya Kiisilamu, matarajio ya kitamaduni na mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia vikionekana kuwa nguzo kuu za kumjenga/kumdidimiza mwanamke katika jamii ya kisasa.Makala yanahitimisha kuwa shairi la *Mahavule na Jamii* linajenga taswira ya mwanamke inayojaribu kuoanisha heshima na utambulisho wa kidini na mahitaji ya ushiriki wake katika jamii ya kisasa. Mwanamke anapewa nafasi kubwa katika jamii na maendeleo yanayotegemea pakubwa uwajibikaji wake. Makala hii inatoa mchango muhimu katika fasihi hasa ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu kwa kudhihirisha jinsi dini, utamaduni na mabadiliko ya kiwakati vinaweza kutumiwa na watunzi kwa pamoja kumjenga mwanamke na kuijenga nafasi yake katika jamii ya sasa.

Maneno Muhimu: Mwanamke, usasa, taswira, ufeministi wa Kiisilamu, ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu.

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

UTANGULIZI

Changamoto kubwa inayoukabili ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu wa kisasa ni namna ya kusawiri taswira ya mwanamke katika mazingira yanayokabiliwa na kasi kubwa ya mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kielimu na kiteknolojia. Wakati mapito ya kiwakati, mifumo ya kidijitali na utandawazi ikileta mitazamo mipya kuhusu uhuru, majukumu, na nafasi ya mwanamke katika ulimwengu wa sasa, watunzi wengi wa ushairi wa kisasa wanajikuta katika mzozo wa kiitikadi. Kasi ya teknolojia na utandawazi imetikisa misingi mingi ya kijamii, ikilazimisha fasihi ya Kiswahili kutafuta lugha mpya ya uwakilishi wa kijinsia. Mzozo huu unahusisha mvutano kati ya kuhifadhi misingi thabiti ya kidini na maadili ya kijadi ya mwanamke wa Kiisilamu, dhidi ya kuakisi uhalisia wa mwanamke wa sasa ambaye anashiriki kikamilifu katika elimu ya kisasa, ajira, na matumizi ya teknolojia.

Licha ya kuwepo kwa changamoto hizi katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu, kihistoria, utanzu huu umekuwa miongoni mwa tanzu za fasihi zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika kuhifadhi, kuendeleza na kusambaza amana za kijamii, kidini na kitamaduni za Waswahili. Utanzu huu umekuwa na uhusiano wa karibu na Uisilamu, hususan kutokana na mwingiliano wa kihistoria na kiutamaduni kati ya jamii za Waswahili na Waarabu katika ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki. Mwingiliano huo ulichangia kuibuka na kukua kwa utamaduni wa kishairi uliobeba athari za dini ya Uisilamu, huku ukiendelea kujidhihirisha kupitia lugha, mitindo na maudhui yanayohusiana na mazingira ya Waswahili. Taib (2021) anaeleza kuwa ingawa ushairi huu uliathiriwa na kaswida za Kiisilamu za Kiarabu, uliweza kuingizwa katika mazingira ya Waswahili na kuendelezwa kwa namna iliyoufanya kuwa sehemu muhimu ya utamaduni wao wa kifasihi. Aidha, maendeleo ya ushairi huu yalichangia kuibuka kwa tungo zilizobeba maudhui ya kidini, kijamii na kiutamaduni ambazo zilitumiwa pia kuwasilisha, kujadili na kuhakiki masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii, yakiwemo ya usawiri wa mwanamke na nafasi yake katika mifumo ya kijinsia.

Kadhalika, uhusiano huu kati ya utamaduni wa Waswahili na Uisilamu umechangia kuibuka kwa kazi maarufu za kale zinazojadili nafasi ya mwanamke. Mazrui (2007) anajadili nafasi ya mwingiliano wa tamaduni katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili ambapo kazi kama Utenzi wa *Mwana Kupona na Utenzi wa Fatuma* zilichukua nafasi muhimu ya kutumia ushairi kuwasilisha mafunzo kuhusu nafasi, wajibu na mwenendo unaotarajiwa kwa mwanamke. Kazi hizi ziliunganisha misingi ya kidini na matarajio ya kitamaduni katika kumwelekeza mwanamke kuhusu maisha ya ndoa na familia.

Hata hivyo, kuendelea kutegemea tenzi hizi za kijadi kama mifano mikuu ya kuchunguza suala hili kunaacha pengo kubwa katika uelewa wa namna mwanamke wa kisasa anavyowakilishwa. Nafasi mpya ya mwanamke katika mazingira ya sasa ya kidijitali haiwezi kufungwa tena ndani ya kuta za nyumbani tu, kwani mwingiliano wa kijamii umetanuka nje ya mipaka ya kijadi. Tenzi hizo za kikale zimeishia tu kumwelekeza mwanamke katika mazingira ya nyumbani (ndani) na kukosa kuieleza nafasi yake katika jamii pana ambayo imepitia mabadiliko makubwa ya kiteknolojia na kiuchumi. Changamoto hii inaleta umuhimu wa kuchunguza ushairi wa kisasa ili kuona namna watunzi wanavyolishughulikia suala la mwanamke kwa kuakisi mazingira haya mapya.

Kwa kuzingatia muktadha huo, makala haya yanachunguza taswira ya mwanamke katika shairi la *Mahavule na Jamii* la Mahmoud Ahmed Abdulkadir, maarufu kama Ustadh Mau. Uchunguzi huu unalenga kubainisha namna mtunzi anavyomwakilisha mwanamke katika miktadha mbalimbali ya maisha ya kisasa na kuchunguza itikadi za kijamii na kidini zinazojitokeza kupitia usawiri huo, huku yakitathmini namna taswira hizo zinavyoweza kufasiriwa. Sehemu zinazofuata zimeangazia: msingi wa nadharia ambapo misingi ya nadharia ya Ufeministi wa Kiisilamu imeeleza jinsi ilivyoongoza uchanganuzi; ufafanuzi wa mbinu za utafiti kutoka kwa mtunzi kupitia usampulishaji kimakusudi na mahojiano pamoja na uchanganuzi wa taswira za mwanamke katika shairi teule ambazo ni nguzo ya maadili na stara, kiumbe tukufu, moyo wa familia, mhusika shupavu na mwanaharakati na kioo cha changamoto za kisasa.

MAPITIO YA MAANDISHI

Taswira ya mwanamke ni suala ambalo limejadiliwa kwa muda mrefu katika taaluma ya fasihi. Hali hii inatokana na nafasi muhimu anayoshikilia mwanamke katika jamii pamoja na namna anavyowakilishwa kupitia kazi mbalimbali za kifasihi. Mulokozi (1996) anadai kuwa utanzu wa kwanza kabisa katika ulimwengu wa fasihi ni ushairi ambao ndio pia ulioanza kumsawiri mwanamke katika hali tofautitofauti. Taswira ya mwanamke katika

jamii hivyo ni suala kongwe ambalo limeangaziwa katika tanzu mbalimbali za fasihi ukiwemo ushairi. Kama anavyoeleza Senkoro (1982) taswira ni mkusanyiko wa picha mbalimbali ziundwazo na maelezo ya wasanii katika kazi ya fasihi. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa ni mkusanyiko wa picha anazopata msomaji au msikilizaji baada ya kusoma, kuona au kusikiliza kazi ya fasihi.

Kwa kuzingatia mitazamo hiyo, taswira ya mwanamke katika fasihi inaweza kueleweka kama mkusanyiko wa picha, mitazamo na dhana ambazo mtunzi hujenga kuhusu utambulisho, uwezo, nafasi na majukumu ya mwanamke katika jamii. Taswira hizi zinaweza kuwa chanya au hasi kutegemea itikadi, mazingira na msimamo wa mtunzi. Vilevile, zinaweza kuendeleza mitazamo iliyopo katika jamii au kuibua mitazamo mipya inayopinga mifumo ya kijamii inayomdunisha mwanamke. Usawiri wa mwanamke katika makala haya umezidi kutilia mkazo kauli inayosema kuwa fasihi haitoki katika ombwe tupu. Mjadala kuhusu taswira ya mwanamke katika jamii imeangaziwa na wanafasihi wengi katika nyakati mbalimbali za maisha ya mwanadamu na katika tanzu mbalimbali za fasihi. Huku wengi wakiwa na nia ya kutoa mwanga juu ya suala hili, wengi wanaishia kuweka bayana uhalisia wa nafasi za wanawake katika utamaduni asilia.

Ekiru (2026) alichunguza usawiri wa Fatuma kama kielelezo cha shujaa wa Kiisilamu kwa kurejelea *Utenzi wa Fatuma*. Makala hii ililenga kuonyesha nafasi ya mwanamke katika masuala ya kishujaa kwa kurejelea mhusika Fatuma kupitia namna alivyowasilishwa katika kazi teule kuonyesha ushujaa wa mwanamke katika muktadha wa Kiisilamu na namna anavyotumika kama mfano wa kuigwa na wanawake. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha jinsi Fatuma ni mfano wa mwanamke shujaa ambaye katika kujitolea kwake katika masuala ya kidini, kifamilia na kijamii alifanikiwa katika kuendeleza haki, usawa na ustawi wa wanawake Waisilamu. Ekiru alitumia mhusika huyu pia kuonyesha nafasi muhimu ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili na kuchangia pia katika ukuzaji wa mtazamo mpya wa wanawake katika fasihi na jamii kwa ujumla. Utafiti huu ulikuwa muhimu katika makala haya kwa sababu uliangazia namna mwanamke alivyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu. Hivyo basi ilimsaidia mtafiti katika uelewa na ubainishaji wa taswira na mbalimbali za mwanamke kwa kurejelea tungo za kidini pamoja na mitazamo mipya ya wanawake katika tungo za Kiisilamu. Huku utafiti huu ukizingatia utenzi wa kishujaa wa kimapokeo kushughulikia taswira maalumu ya ushujaa, utafiti wetu ulipiga hatua zaidi kwa kushughulikia ushairi wa kisasa na taswira mbalimbali za wanawake katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu na sio taswira moja tu.

Naye Balisidya (1982), alichunguza taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi ya Tanzania kwa kurejelea hadithi fupi, vitendawili na nyimbo. Utafiti wake ulionyesha kuwa usawiri wa mwanamke katika fasihi simulizi unahusishwa kwa karibu na mifumo ya kitamaduni ya jamii. Mwanamke alisawiriwa katika nafasi mbalimbali, zikiwemo za mlezi wa familia na chombo cha starehe kwa mwanamume. Mchango wa utafiti huu ni kubainisha namna itikadi za kijamii zinavyoathiri uwakilishi wa mwanamke katika kazi za kifasihi. Utafiti wa Balisidya (1982) ulikuwa na mchango katika kazi hii kwa namna ambavyo matokeo yake yalidhihirisha jinsi itikadi na mifumo ya kitamaduni ndiyo inayofafanua majukumu na uwakilishi huo wa mwanamke, hivyo kumsaidia mtafiti kuelewa umuhimu wa masuala ya kitamaduni katika ugavi na uwakilishi wa majukumu ya mwanamke katika jamii. Hata hivyo, utafiti huo ulijikita katika fasihi simulizi huku utafiti wetu ukijikita katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu na kuangazia kwa kina mabadiliko ya taswira ya mwanamke hivi leo.

Kwa upande mwingine, Kioko na wenzake (2025) alichunguza usawiri wa mwanamke wa kisasa wa Kiisilamu katika filamu ya Maria. Utafiti huu ulilenga kubainisha nafasi ya mwanamke wa Kiisilamu katika jamii na namna anavyowakilishwa kupitia taswira chanya na hasi. Matokeo yalidhihirisha kuwa mwanamke anaweza kusawiriwa kama mlezi, mkombozi na mhusika mwenye uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii, licha ya kukabiliwa na changamoto zinazotokana na mfumo dume. Kioko na wenzake (2025) waliweza kuonyesha namna mwanamke wa Kiisilamu ana nguvu ya kuleta mabadiliko katika jamii licha ya kuwa kukabiliwa na changamoto ya mfume dume ambao mara kwa mara hudunisha mchango wake katika jamii. Makala haya yalifaidi katika kazi hii kwa sababu ulimsaidia mtafiti katika kuelewa majukumu mbalimbali ya mwanamke katika jamii na matarajio yake katika kuleta mabadiliko katika jamii. Utafiti wa Kioko na wenzake (2025) ulijikita katika utanzu wa filamu pekee na kuacha kabisa utanzu wa ushairi hivyo kushinikiza utafiti katika ushairi

wa Kiswahili wa Kiisilamu katika makala haya kwa lengo la kuziangazia taswira hizi za wanawake.

Katika utafiti mwingine, Momanyi (2012) alichunguza usawiri wa mwanamke Muisilamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili kwa kurejelea kazi za Muyaka bin Haji, Mwanakupona Binti Mshamu na Shaaban Robert ili kubaini jinsi mwanamke alivyosawiriwa. Kupitia kazi kama Mwanakupona uchunguzi huu ulibainisha jinsi mwanamke anavyojitokeza kulingana na itikadi kupitia uainishaji wa majukumu yake katika utenzi huu hivyo kutuwezesha kuona picha halisi ya mwanamke katika kipindi hicho. Aidha, kupitia shairi la Shaaban Robert aliweza kubaini taswira ya mwanamke na nafasi aliyotengewa na jamii kwa kujadili msimamo wa mwandishi kuhusu suala la mwanamke kulingana na mabadiliko yaliyoikumba jamii ya wakati wake. Kupitia kazi hizo, Momanyi alibainisha nafasi mbalimbali alizotengewa mwanamke na jamii, pamoja na namna mabadiliko ya kihistoria yalivyoathiri mitazamo ya watunzi kuhusu mwanamke. Utafiti huu ulikuwa muhimu kwa makala haya kwa sababu ulimsaidia mtafiti katika kuvielewa vipengele vya kihistoria, kiitikadi na mabadiliko ya kijamii na jinsi vinaathiri mitazamo ya watunzi kuhusu nafasi na majukumu ya wanawake katika jamii husika. Huku utafiti huu wa Momanyi ukijikita katika ushairi wa Kiswahili katika kusawiri taswira za mwanamke wa Kiisilamu, utafiti wetu ulijikita katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu wa kisasa katika usawiri wa taswira za mwanamke Muisilamu.

Kwa ujumla, tafiti hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa kuelewa namna mwanamke anavyowakilishwa katika tanzu mbalimbali za fasihi. Kazi hizi zimetumiwa na mtafiti ili kuelewa kwa upana suala hili kwa uga mpana ukigusia fasihi simulizi, maonyesho (filamu) na hata andishi. Hata hivyo, bado kuna umuhimu wa kupanua mjadala huo kwa kuchunguza ushairi wa Kiswahili wa Kiislamu wa karne ya ishirini na moja. Tofauti na tafiti zilizotangulia, makala haya yanajikita katika shairi la *Mahavule na Jamii* ili kuchunguza namna mtunzi wa kisasa anavyomwakilisha mwanamke katika muktadha wa mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia. Hivyo, makala haya yanachangia kupanua mjadala kuhusu mwendelezo na mabadiliko ya taswira ya mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu.

Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yaliongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Kiisilamu. Nadharia hii inachunguza masuala ya haki, usawa, heshima na nafasi ya mwanamke kwa kuzingatia misingi ya mafundisho ya Kiisilamu. Ufeministi wa Kiisilamu uliibuka katika miaka ya 1890 kama harakati ya mabadiliko katika urazini wa watu wenye mizizi yake katika usawa wa waisilamu wote, wake kwa waume, mahali popote hadharani au faraghani (Noordin 2006). Mizizi ya mijadala ya kisasa ya Ufeministi wa Kiisilamu inahusishwa na harakati za mageuzi ya kijamii na kielimu zilizojitokeza katika ulimwengu wa Kiisilamu, hususan Misri, mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Mijadala hii ikigusia masuala mbalimbali yakiwemo mavazi, elimu, unyumba, vyama na sera za ufeministi za wanawake wa Kiarabu. Wanamageuzi (Lord Croner,1901; al- Tahtani, 1801; Amin 1899;) walichangia mijadala hiyo kwa kutetea umuhimu wa elimu na mageuzi ya kijamii. Hata hivyo, Ufeministi wa Kiisilamu kama mkabala wa kisasa ulijitokeza na kuimarika zaidi katika miaka ya 1980 na 1990.

Ahmed (1992) anajadili historia ya mitazamo kuhusu wanawake na jinsia katika jamii za Kiisilamu Misri kwa kuonyesha namna mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa nchini humo baada ya mkoloni Muingereza kuitawala Misri yalileta matatizo ya wanawake kupelekea masuala ya wanawake kuanza kuhusishwa kwa masuala ya kitabaka, kitaifa, kitamaduni na kisiasa tofauti na awali ambapo mwanamke alifungika na kazi za nyumbani tu.

Noordin (2006), anaendeleza nadharia hii kwa kuuhusisha Ufeministi wa Kiisilamu na mwamko wa wanawake katika masuala ya kidini, kijamii na kiutamaduni kwa kuzingatia misingi ya Kurani na Sunna. Mtazamo huu unasisitiza kuwa haki na hadhi ya mwanamke zinapaswa kutazamwa kwa kuzingatia mafundisho ya Kiisilamu badala ya kutegemea mila na desturi ambazo zinaweza kupingana na misingi ya uadilifu wa dini hiyo.Tofauti na Ufeministi wa Kimagharibi, Ufeministi wa Kiisilamu umepiga hatua mbele kwa sababu, wakati ambapo Ufeministi wa Kimagharibi ulidai haki ya mwanamke katika nyanja za umma-kazini, elimu na kadhalika, Ufeministi wa Kiisilamu umedai haki hizo na uadilifu kwa mwanamke mpaka nyumbani kwake. Nadharia hii hivyo hulenga katika kumkomboa mwanamke na kumwangalia kwa heshima, usawa, haki na taadhima kupitia maandiko ya Kurani tukufu, Sunna na misingi ya sheria za Kiisilamu. Huku jamii nyingi za Kimagharibi na zile zisizokuwa na Kiisilamu kuonelea kwamba mwanamke wa Kiisilamu

anakandamizwa kupitia njia mbalimbali, misingi ya nadharia hii imemsaidia mtafiti kuelewa namna dini ya Kiisilamu imemwezesha mwanamke kupitia mafundisho ya Kurani na Sunna.

Ekiru (2026) anadai kuwa kwa misingi ya Kurani na Sunna, Uisilamu unasisitiza kwamba wanawake hawakupangiwa kuwa wanyonge au wasio na mamlaka bali washiriki madhubuti katika jamii za Kiisilamu. Ekiru (keshatajwa) ameorodhesha mihimili mitano ya nadharia hii kama ifuatavyo:
Ufasiri sahihi wa Kurani na Sunna
Ukombozi kupitia imani
Uadilifu wa kijamii na kimaadili
Kupinga mfumo dume wa kitamaduni
Usawa wa kiroho

Mtafiti aliamua kuacha mhimili wa tano na kutumia mihimili minne ya kwanza kwa sababu ya uwazi wake katika kutafsiri na kuchanganua masuala mbalimbali kama mwingiliano wa kiitikadi kati ya maandiko ya kidini, tafsiri za kijinsia, utamaduni, nafasi na mamlaka ya mwanamke katika jamii na ulimwenguni kwa jumla.

MBINU ZA UTAFITI

Buliba na wenzake (2014) wanasisitiza kwamba kwa asilimia kubwa tafiti zinazohusu lugha, isimu na fasihi ni za kimaelezo. Utafiti huu hivyo ulichukua mkabala wa kimaelezo kwa kuwa ulilenga kuchunguza taswira ya mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu wa karne ya 21 hivyo kumpa mtafiti nafasi ya kutoa maelezo ya kina kuhusu taswira ya mwanamke katika shairi teule.

Data ilikusanywa nyanjani katika eneo la Lamu. Eneo hili liliteuliwa kimakusudi kwa sababu ya mchango wake mkubwa katika historia ya chimbuko la mashairi ya Kiswahili ya Kiisilamu hivyo kurahisisha upatikanaji wa watunzi wa mashairi haya. Mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi kupata watunzi wa mashairi ya Kiswahili ya Kiisilamu na mashairi yenyewe. Katika usampulishaji huu mtafiti alifanikiwa kupata mtunzi Mahmoud Abdulkadir kwa sababu ya umaarufu wake wa utunzi wa mashairi ya kidini. Kutoka kwa mtunzi huyu mtafiti alitumia mbinu ya mahijiano kukusanya mashairi matano na akaamua kutumia moja (*Mahavule na Jamii)* kwa sababu lilitungwa kwa ajili ya wanawake hasa mabinti na lilizungumzia masuala ya wanawake kwa upana.

Uchanganuzi wa data ulifuata hatua zilizowekwa na Oso na Onen (2005). Hatua hizi zinahusisha upangaji wa data husika, uchanganuzi wa data kulingana na malengo na maswali ya utafiti na kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa data kwa manufaa ya msomaji au wahusika wengine katika uwanja tafitiwa. Uchanganuzi ulizingatia hatua hizi muhimu ambapo mtafiti alipanga na kuchanganua data yake kulingana na malengo ya utafiti, kisha kuyawasilisha matokeo kwa maelezo ya kina yaliyoshereheshwa na madondoo/beti kutoka kwa shairi teule. Mtafiti alizingatia maadili kwa kuenda nyanjani baada tu ya kupata kibali cha kufanya hivyo kutoka NACOSTI. Vilevile, aliomba idhini kuhoji mtafitiwa na kutumia kazi yake katika makala ambapo alikubali kuhojiwa na akaridhia kazi yake kutumika katika makala haya.

MATOKEO YA UTAFITI

Uchambuzi wa shairi la *Mahavule na Jamii* unaonyesha kuwa taswira ya mwanamke imejengwa kupitia mvutano na mwingiliano wa kiitikadi kati ya misingi ya kidini, matarajio ya kitamaduni na mabadiliko ya kijamii yanayojitokeza katika ulimwengu wa kisasa. Kupitia uteuzi makini wa lahaja ya Kiamu, marejeleo ya kihistoria ya wanawake mashujaa wa Kiisilamu, na jazanda nzito, mtunzi Mahmoud Ahmed Abdulkadir (Ustadh Mau) anaunda taswira kuu tano za mwanamke: nguzo ya maadili na stara, kiumbe mtukufu, moyo wa familia, mhusika shupavu na mwanaharakati, pamoja na kioo cha changamoto za kisasa. Ujenzi wa taswira hizi unalenga kulinda maadili ya kijadi na taasisi ya familia dhidi ya athari za mitandao ya kijamii, huku ukifichua ukinzani wa kijinsia ambapo utukufu anaopewa mwanamke unaambatana na udhibiti wa mfumo dume unaomtwisha msichana (*havule*) mzigo mkuu wa kulinda heshima ya jamii.

Mwanamke kama Nguzo ya Maadili na Stara

Hii ni taswira ya kijadi na yenye nguvu zaidi katika ushairi huu na mtunzi ameindeleza mpaka katika mashairi ya sasa. Katika shairi la *Mahavule na Jamii*, mwanamke anasawiriwa kama nguzo ya kudumisha na kuendeleza maadili ya kidini na kijamii. Taswira hii inajitokeza kupitia msisitizo wa mtunzi kuhusu umuhimu wa heshima, stara na mwenendo mwema. Mtunzi anawalenga hasa mabinti kwa kuwahimiza kuzingatia maadili yanayokubalika katika jamii ya Kiisilamu. Kwa kufanya hivyo, anajenga dhana kuwa mwenendo wa mwanamke una uhusiano wa karibu na ustawi wa familia na jamii kwa ujumla.

Kwanza, mwanamke anasawiriwa kama mlinzi wa maadili ya familia na jamii kulingana na mafundisho ya Kiisilamu. Mtunzi katika ubeti wa 13 unahusia mabinti kuitukuza heshima ili wawe watu wema waweze kuiongoza jamii. Mtunzi anamchora mwanamke aliye na heshima kama yule aliyetukuka na mwenye daraja ya juu katika jamii yake hivyo kuwa na imani naye hata katika kuiendesha au kuiongoza jamii yake vizuri. Tazama ubeti wa 13 mtunzi anaposema:

Iwekeni hishima muithukuze
Muwe wachu wema jamii muiongoze
Pache hawave nao asiwapuze
Wala kwenye upochofu wasiwaekeve.

Katika ubeti huu, mshororo "*Muwe wachu wema jamii muiongoze*" unadhihirisha matarajio ya mtunzi kwamba mwanamke mwenye maadili ana uwezo wa kuwa kiongozi na mshiriki muhimu katika maendeleo ya jamii. Hapa, mwanamke hachorwi kama mtu anayepaswa kufuata maelekezo pekee, bali kama mhusika mwenye wajibu wa kuathiri mwelekeo wa jamii kupitia tabia na mwenendo wake. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiisilamu, usawiri huu unahusiana na mhimili wa uadilifu wa kijamii na kimaadili. Mtunzi anatambua kuwa mwanamke ana nafasi muhimu katika kujenga jamii yenye misingi ya maadili.

Aidha, mtunzi anaunganisha suala la maadili na stara ya kimavazi. Stara hii ya mavazi haitazamwi kama kizuizi, bali kama alama ya heshima, utambulisho, na ulinzi dhidi ya maovu ya kijamii. Mtunzi anawahusia mabinti katika stara kwa hofu ya kutapakaa kwa uovu na ulanisi katika jamii kutokana na kutokuwa na mipaka ya suala stara katika ulimwengu wa sasa. Ubeti huu unaonyesha namna mtunzi anavyotafsiri mabadiliko ya kisasa kama chanzo cha changamoto zinazohusiana na maadili. Maneno "hishima na stara" yanasisitiza kuwa heshima ya mwanamke inahusishwa na mwenendo wake pamoja na namna anavyojisitiri. Mtunzi anatumia lugha ya tahadhari na ukemeaji kuonya dhidi ya tabia anazoziona kuwa zinazokinzana na misingi ya maadili ya Kiisilamu. Tazama ubeti wa 16.

Ni ulimwengu wa ushethwani kuubarikia
Hishima na stara hazina maridhia
Uvundo na ulanisi hutukudhwa
Si dunia milanyndo na tabia khudhia.

Mtunzi ameambatisha suala la sitara ya tabia na sitara ya mavazi kwa kukokotezea uvaaji bora miongoni mwa wanawake katika jamii yake. Suala la mavazi analiona kama chanzo cha kuiharibu dunia yao. Tazama ubeti wa 17.

Kuvaa bora ni kudhia
Kuvaa dufu ni kusuluhia
Haya ndio adhakao kuchuia
Kuchuharibia yechu dunia.

Kupitia ubeti huu, mtunzi anaweka mavazi katika nafasi ya alama ya utambulisho wa kijamii na kidini. Kwa mtazamo wake, mavazi si suala la urembo pekee bali pia ni kipengele kinachohusiana na heshima na maadili. Mwanamke anayezingatia stara anajengwa kama kielelezo cha mwanamke mwenye hadhi na anayeheshimika katika jamii.

Hata hivyo, uchambuzi wa kina unaonyesha mvutano kati ya kumtambua mwanamke kama mhusika mwenye uwezo wa kuongoza jamii na kumfanya awajibike kwa kiasi kikubwa kulinda maadili kupitia mavazi na tabia zake. Taswira hii inaoana na ile ya Kioko na wenzake (2025) kuhusu mwanamke wa kisasa kwamba licha ya yeye kukabiliwa na changamoto za kijamii ana uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii. Hivyo, taswira hii inadhihirisha namna ushairi wa Kiisilamu wa kisasa unavyojaribu kuoanisha matarajio ya kidini na nafasi ya mwanamke katika jamii inayobadilika.

Mwanamke kama Kiumbe Tukufu

Taswira nyingine inayojitokeza katika *Mahavule na Jamii* ni mwanamke kama kiumbe mwenye hadhi na utukufu mkubwa katika mtazamo wa Kiisilamu. Utukufu huu katika misingi ya Ufeministi wa Kiisilamu umejikita katika kumwekea mwanamke heshima, usawa, uadilifi na hadhi sambamba na viumbe wengine. Mtunzi anatumia marejeleo ya mafundisho ya kidini na historia ya Uisilamu kuthibitisha nafasi ya mwanamke katika jamii. Kupitia mbinu hii, anajenga hoja kuwa mwanamke hastahili kudunishwa kwa misingi ya jinsia yake, bali anatakiwa kuheshimiwa kutokana na hadhi aliyopewa na Mwenyezi Mungu. Katika ubeti wa 2 wa shairi hili mtunzi anaeleza utukufu wa mwanamke na daraja aliyokuwa nayo katika maisha ya mwanadamu kulingana na dini ya Kiisilamu. Katika ubeti wa pili kama inavyodhihirika hapa chini, mtunzi anarejelea kauli ya Mtume kuonyesha utukufu na daraja tatu alizopewa mwanamke kabla ya mwanamume katika dini ya Kiisilamu. Hivyo naye anaendeleza kumtukuza mwanamke katika kazi yake kama ilivyo katika dini ya Kiisilamu.

Humswalia wechu nchume
Alonena aheshimiwe mame
Mara chachu awake mume
Na kumtukuza nisikome.

Ubeti huu unasisitiza heshima anayostahili kupewa mama katika familia na jamii. Mtunzi anarejelea mafundisho yanayohusishwa na Mtume kuhusu umuhimu wa kumheshimu mama. Kwa kufanya hivyo, anatumia mamlaka ya kidini kujenga taswira ya mwanamke kama mtu mwenye hadhi na anayestahili kutukuzwa.

Kwa kuendelea, mtunzi katika ubeti wa 10 anajaribu kutoa taswira ya utukufu na uongofu wa mwanamke kupitia ushahidi wa kihistoria wa wanawake wa awali katika Uisilamu. Ubeti huu unaonyesha thamani ya mwanamke wa Kiisilamu kupitia wanawake watatu katika historia ya Uisilamu wakiwemo (Nana Hadija, Sumeya na Asia). Ushujaa walioonyesha wanawake hawa katika Uisilamu umetumiwa na mtunzi kama kigezo cha kuhamasisha mabinti wa sasa kutobakia nyuma katika masuala ya kijamii. Kumbukumbu ya historia za wanawake hawa zimetumiwa kuonyesha imani kubwa ya Nana Hadija mpaka kumfanya yeye kuwa mwanamke wa kwanza kuamini katika Uisilamu, ushujaa wa Bi. Sumeya kufa akiwa shahidi wa kwanza katika Uisilamu na maamuzi ya Bi. Asia kumpinga mumewe Firauni zimetumiwa kuonyesha pia namna wanawake ni watu wenye imani, maamuzi, ushujaa na mamlaka katika jamii. Hii inawapa mabinti fursa ya kuwajibika kikamilifu katika ujengaji jamii na dunia kwa ujumla. Tazama ubeti wa 10.

Wa kwandha kuamini wendani
Wa kwandha kufa shahidi uisilamuni
Wa kwandha kuupinga ufirauni
Ni wanawake hawa chusisahauni.

Marejeleo ya wanawake hawa yanadhihirisha matumizi ya historia kama nyenzo ya kuhalalisha na kuimarisha hadhi ya mwanamke katika jamii ya sasa. Mtunzi anatumia mifano ya wanawake waliokuwa na mchango mkubwa katika historia ya Uisilamu kuwahamasisha wanawake wa kizazi cha sasa kutambua uwezo wao na kushiriki katika masuala ya kijamii na kidini. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiisilamu, mfano huu unaendana na mhimili wa ukombozi kupitia imani. Mtunzi anatumia historia ya kidini kuonyesha kuwa imani si kikwazo cha maendeleo ya mwanamke, bali inaweza kuwa msingi wa kumwezesha kushiriki katika shughuli za kijamii na kujenga utambulisho wenye hadhi. Taswira hii inaendeleza ukuzaji wa mtazamo mpya wa wanawake katika mashairi ya Kiswahili ya Kiisilamu Ekiru (2026).

Aidha, mtunzi ameuzungumzia utukufu wa mwanamke katika ubeti wa 28 na 29 kwa kutueleza namna Mwenyezi Mungu alimchagua mwanamke kuwa mama wa ulimwengu wake dhidi ya mwanamme. Uchaguzi huu unarejelewa na mtunzi kama mapenzi ya Mungu kwa mwanamke na kumtukuza. Katika ubeti huu, mwanamke anahusishwa na nafasi ya umama na jukumu la kuendeleza uhai wa jamii. Mtunzi analitumia jukumu hili kama msingi wa kuthibitisha utukufu wa mwanamke. Vilevile katika ubeti wa ishirini na tisa tunaonyeshwa upekee wa mapenzi haya kwa kuelezwa jinsia katika Kurani Tukufu iliyo na sura 114 hakuna sura ya wanaume bali ya wanawake tu kwa ajili ya kumtukuza mwanamke. Tazama ubeti wa 28 na 29 mtawalia.

Mungu alimchagua mwanamke
Awe mama wa ulimwengu wake
Haya mapendhi ya mola yafahamike
Kwa kumfanya mwanamke atukuke.
Mswahafuni suratunisai mia
Waisilamu walichuchumia
Hakuna suraturijali nawambia
Ni kuwatukuza ini hundhasikia.

Mafunzo haya yanayotokana na kauli za Mtume (sunna) na maneno ya Mwenyezi Mungu kutoka kwa Kurani Tukufu yametumiwa na mtunzi kuonyesha taswira ya utukufu wa mwanamke mbele ya viumbe watukufu (Mtume na Mungu) kabla hata ya mwanadamu mwenzake. Kurani na Sunna zimetumika kufasiri kwa usahihi nafasi ya mwanamke kama ilivyojadiliwa katika Kurani na Sunna za Bwana Mtume. Kwa jumla, kupitia marejeleo ya kidini na kihistoria, mtunzi anajenga taswira ya mwanamke kama kiumbe mwenye hadhi ya kipekee. Taswira hii inatoa changamoto kwa mitazamo inayomdunisha mwanamke na inasisitiza umuhimu wa kumtambua kama mshiriki muhimu katika maisha ya kidini na kijamii.

Mwanamke kama Moyo wa Familia

Katika *Mahavule na Jamii*, mwanamke anasawiriwa pia kama kiini cha familia kupitia nafasi yake ya uzazi, malezi na uendelezaji wa mahusiano ya kifamilia. Mtunzi anaweka msisitizo katika mchango wa mwanamke katika kulea watoto, kuheshimu wazazi na kuendeleza maadili ya familia. Taswira hii inaonyesha kuwa familia ni

mojawapo ya maeneo muhimu ambayo kupitia kwayo hadhi na wajibu wa mwanamke vinajengwa.Mtunzi ameizungumzia taswira hii katika ubeti wa 43 kwa kurudia kauli "*Mwanamke ni*" kuonyesha nafasi mbalimbali za mwanamke katika mfumo wa kifamilia. Urudiaji huu unasisitiza kuwa mwanamke ni mama, mtoto na mlezi mwenye mchango mkubwa katika kudumisha uhusiano wa kifamilia. Aidha, unajenga mtazamo kuwa mwanamke anashiriki katika mzunguko wa maisha ya familia kupitia nafasi mbalimbali anazozitekeleza.

Mwanamke ni mame alinizaa na kunilea
Mwananke ni mwanangu heshima kuniwekea
Mwananke ni wana walionidhalia
Mwananke ni wangu udhuri kunitakia.

Kadhalika mtunzi amemjengea mwanamke taswira ya utukufu katika familia kwa kueleza nafasi na uwezo alionao kwa jamii yake. Mbali na kumsisitizia heshima anatambuliwa kama mlezi wa imani katika jamii. Mtunzi anaeleza namna pepo iko chini ya wayo za akina mama hivyo kuhimiza watoto waheshimu wazazi ili wapate pepo. Yeye ni kioo cha malezi bora ya kijamii na kidini nyumbani. Tazama ubeti wa 45 na 47 mtawalia.

Ndio hawa mahavule kuwaambia
Utukufu wa mwananke kunthakia
Mledhi wa jamii katika dunia
Athukuao mimba miezi tisia.
Mwananke ndiye aloniacha duniani
Kwa maamrisho ya Mola Rahamani
Tuko tini ya nyayo zake mlango wa peponi
Ndio kawambia mahavule ihishimuni.

Mtunzi anaendeleza taswira hii katika beti zilizotangulizwa hapo juu kwa kuhusisha nafasi ya mama na mafundisho ya Kiislamu kuhusu heshima kwa wazazi. Kauli "Tuko tini ya nyayo zake mlango wa peponi" inasisitiza nafasi ya mama katika mafundisho ya Kiislamu kuhusu wema kwa wazazi. Mtunzi anatumia rejeleo hili la kidini kuhamasisha heshima kwa wanawake, hususan akina mama, na kutambua mchango wao katika malezi na ustawi wa familia. Kwa kuzingatia Ufeministi wa Kiisilamu, taswira hii inahusiana na mhimili wa uadilifu wa kijamii na kimaadili. Mwanamke anapewa hadhi katika familia na mchango wake unatambuliwa kama sehemu muhimu ya ustawi wa jamii. Usawiri huu umeweza kuonyesha namna matarajio ya kijinsia yanavyoendelea kujitokeza katika ushairi wa Kiswahili wa Kiislamu wa kisasa.

Mwanamke kama Mhusika Shupavu na Mwanaharakati

Shairi la *Mahavule na Jamii* limemwakilisha mwanamke kama mhusika mwenye uwezo wa kushiriki katika shughuli za maendeleo ya kijamii na kielimu. Sawia na kazi ya Momanyi (2012) makala haya yameweza kudhihirisha jinsi mabadiliko ya kihistoria yalivyoathiri mitazamo ya watunzi kuhusu wanawake. Mtunzi anatambua mabadiliko yanayotokea katika jamii ya sasa na umuhimu wa mwanamke kupata elimu na kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ya jamii. Mwanamke anahimizwa kutafuta elimu. Na si elimu ya dini tu, bali pia elimu ya dunia (sayansi, teknolojia, nk.). Mtunzi anaeleza umuhimu wa mwanamke wa sasa kuitafuta elimu kwa manufaa yake yeye mwenyewe na jamii yake. Katika ubeti wa 33 anaweka wazi manufaa ya elimu kwa mwanamke na kwamba kuitafuta elimu ni kumweka kimaisha na anawahimizi wasiachwe nyuma kamwe. Mwanamke msomi anatazamwa kama mkombozi wa jamii yake. Tazama ubeti wa 33:

Ilimu kalitafuteni
La dunia na dini
Nima musibakieni
Jamii isaidieni.

Ubeti huu unaweka wazi msimamo wa mtunzi kuhusu umuhimu wa elimu kwa mwanamke. Kauli "*La dunia na dini*" inaonyesha kuwa mtunzi anatambua umuhimu wa elimu ya kidini na elimu ya kawaida katika kumwezesha mwanamke kushiriki kikamilifu katika jamii. Matumizi ya neno "*musibakieni*" kwa upande mwingine linaashiria wito wa kutokubaki nyuma katika maendeleo ya kielimu. Hivyo, mwanamke anachorwa kama mhusika mwenye uwezo wa kujifunza, kujitambua na kuchangia maendeleo ya jamii. Hii ni taswira inayopingana na mitazamo inayomwekea mwanamke mipaka katika upatikanaji wa elimu. Kwa mtazamo wa Ufeministi wa Kiisilamu, usawiri huu unaendana na mhimili wa ukombozi kupitia imani. Elimu inachukuliwa kama nyenzo ya kumwezesha mwanamke kutambua haki na wajibu wake, kuimarisha uwezo wake na kushiriki katika maendeleo ya jamii.

Aidha, mtunzi anagusia matumizi ya mitandao ya kijamii kama nyenzo ya kuendeleza elimu na utamaduni. Mtunzi anahimiza mabinti kutumia mitandao kwa ajili ya manufaa yao. Anawasihi kuitumia mitandao ya kijamii kwa manufaa na sio upotovu. Anatambua umuhimu wa mitandao hii kwa ulimwengu wa sasa hivyo kuwashinikiza wanawake kuitumia kujiendeleza na

kujifaidi. Mtunzi ametumia shairi lake kuonyesha na kutetea haki ya wanawake kupata elimu sawia na wakiume. Katika ubeti wa 24 hapa chini mtunzi anawasihi wanawake waingie kwenye mitandao ya kijamii kufunza na kujifunza masuala ya mila, utamaduni na dini. Fursa hii imepewa wanawake kwa kuwa wana uwezo mkubwa wa kuendeleza jambo lolote katika jamii na ulimwengu kwa upana.

Sipeni vishadhi dhahiri simveleve
Ngiani mila yechu muikudhe
Utamaduni wechu muvitukuze
Na dini yechu pache muichangawe.

Katika ubeti huu, mtunzi anawahimiza wanawake kutumia fursa zilizopo katika mazingira ya kisasa kwa kuendeleza mila, utamaduni na dini. Hoja hii inaonyesha kuwa mtunzi hatupilii mbali maendeleo ya kiteknolojia, bali anasisitiza matumizi yake yanayozingatia misingi ya utambulisho wa kidini na kiutamaduni. Kwa hiyo, taswira ya mwanamke kama mwanaharakati inajengwa kupitia uwezo wake wa kutafuta elimu, kutumia teknolojia na kushiriki katika maendeleo ya jamii. Shairi hili hivyo limeweza kuonyesha mabadiliko ya uwakilishi wa mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa Kiislamu wa karne ya ishirini na moja.

Mwanamke kama Kioo cha Changamoto za Utandawazi

Pamoja na kumwakilisha mwanamke kama mhusika mwenye uwezo wa kujiletea maendeleo, mtunzi anaonyesha pia changamoto zinazotokana na mabadiliko ya kiteknolojia na utandawazi. Katika shairi hili, mitandao ya kijamii, mitindo ya mavazi na vyombo vya habari vinawasilishwa kama baadhi ya mambo yanayoweza kuathiri mienendo na maadili ya wanawake katika jamii ya kisasa. Katika shairi la Mahavule na Jamii, mtunzi anaichora taswira ya mwanamke kama aliye katikati ya shinikizo la kuathiriwa na tamaduni za Kimagharibi zinazohimiza "uhuru" fulani wa mavazi na tabia. Katika kazi yake, mtunzi ameonyesha namna utandawazi kupitia maendeleo ya teknolojia kumekuwa umekuwa changamoto kwa watoto wa kike. Matumizi ya mitandao ya kijamii bila mipaka yametajwa pia kama moja ya sababu zinazochangia mmomonyoko wa maadili hasa kwa mtoto wa kike. Mtunzi ameeleza namna mitandao ya kijamii kama vile fesibuku, wasapu, instagramu na tiktok hutumiwa kumdhalilisha na kumshushia hadhi mwanamke katika jamii. Tazama ubeti wa 23:

Ko fesibuku musidanganyike
Uhavule ukakosa udhuri wake
Ngiani kwa akili musihadaike
Kwa mavidio ya ulanisi musihusike.

Katika ubeti huu, mtunzi anatumia majina ya mitandao ya kijamii kutambulisha mazingira mapya ya kijamii yanayowakabili wanawake. Kauli "*musidanganyike*" ni tahadhari inayolenga kuwahimiza mabinti kuwa waangalifu katika matumizi ya teknolojia. Kwa mtazamo wa mtunzi, baadhi ya maudhui yanayosambazwa kupitia mitandao yanaweza kuathiri hadhi na mwenendo wa mwanamke.

Aidha, mtunzi anagusia namna tamaa na vishawishi vya kijamii vinavyoweza kuathiri maamuzi ya mwanamke. Mwanamke amepewa taswira ya kuwa na uwezo wa kushawishika haraka na vitu vidogo vidogo. Mtunzi anawahusia kuchunga uchu wao wasidanganyika na vitu vidogo kama soda, chips na kuku. Fasheni na televisheni vinatajwa pia miongoni mwa mambo yanayofahamika kuwa vishawishi vikubwa vya kutolinda uchu kwa wanawake. Tazama ubeti wa 20.

Kwa soda musiyumbuwe
Kwa kuku na chips musidharauliwe
Fesheni na chivii visiwachafuwe
Kwa Mola wechu ndio chukuelewe.

Ubeti huu unatumia mifano ya vitu vya kawaida katika maisha ya kila siku, kama soda, kuku na chipsi, kuonyesha namna vishawishi vidogo vinavyoweza kuathiri maamuzi ya mtu. Mtunzi anaonya dhidi ya kushawishika kwa manufaa ya muda mfupi na kusahau misingi ya maadili na imani.
Kadhalika mtunzi anaiendeleza taswira hii ya mwanamke kuwa kiumbe dhaifu na mwenye uwezo wa kushawishika katika ubeti wa 21 kwa kuendeleza kusisitiza wawe waangalifu kwenye masuala ya uchu wao ili waendelee kubakia sitarani. Katika ubeti wa 21anasema:

Uchu wechu uchungeni
Mubakie nao sitarani
Sitakeni kuichia aibuni
Kwa kumkuza shetani.

Hapa, matumizi ya kauli "*uchu wechu uchungeni*" yanaonyesha umuhimu wa kujidhibiti na kuwa na msimamo katika maamuzi. Mtunzi anasisitiza kuwa mwanamke anapaswa kujenga uwezo wa kujiongoza na kuepuka vitendo vinavyoweza kuhatarisha heshima yake.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Makala haya yalidhamiria kuchunguza taswira ya mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu wa karne ya ishirini na moja kwa kurejelea shairi la *Mahavule na Jamii* la Mahmoud Ahmed Abdulkadir. Uchunguzi huu umebainisha kuwa usawiri wa mwanamke katika ushairi wa kisasa wa Kiisilamu unajengwa juu ya mwingiliano changamano kati ya mafundisho ya kidini, matarajio ya kitamaduni na mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia.

Matokeo yanaonyesha kuwa mwanamke anasawiriwa katika pande mbili zinazovutana kiitikadi. Kwa upande mmoja, anajitokeza kama kiumbe mwenye hadhi, utukufu, nguzo ya maadili, mhusika shupavu na mshiriki hai katika elimu na maendeleo ya jamii. Kwa upande mwingine, bado anafungwa na wajibu wa kutekeleza matarajio ya kimapokeo yanayohusiana na malezi, stara na udhibiti wa mienendo yake, huku akionekana kama kioo cha changamoto za utandawazi. Mvutano huu unadhihirisha kuwa ushairi wa Kiswahili wa Kiisilamu wa kisasa haujajitenga kikamilifu na misingi ya kimapokeo, bali unajaribu kuoanisha misingi hiyo na mahitaji ya jamii inayobadilika.

Mapendekezo: Makala haya yanatoa mchango muhimu kwa kupanua mjadala wa uhakiki wa kifeministi na ushairi wa Kiisilamu. Utafiti huu unathibitisha kuwa dini si lazima itazamwe kama chombo cha kumkandamiza mwanamke pekee, bali inaweza kutumiwa kama msingi imara wa kutetea heshima, haki na ushiriki wake katika ujenzi wa jamii. Aidha, uchambuzi huu unapendekeza watafiti wa baadaye kuchunguza namna watunzi wa kisasa wanavyotumia lugha ya kishairi kujadili na kusawazisha mipaka kati ya uhuru wa mwanamke na kanuni za kitamaduni na kidini katika zama za utandawazi.

MAREJELEO

Ahmed, L. (1992). *Women and gender in Islam: Historical roots of a modern debate*. Yale University Press.

Amin, Q. (1899). *Taḥrir al-Marʾah (The liberation of women)*. Maktabat al-Taraqqi.

Balisidya, L. (1982). The image of a woman in Tanzania oral literature: A survey. *Journal of Kiswahili Studies, 49*(2), 1–31. https://www.africabib.org/rec.php?RID=184896797&DB=p

Buliba, A., Gwachi, M., & Matinde, R. (2014). *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti*. Serengeti Educational Publishers.

Ekiru, E. S. (2026). Usawiri wa Fatuma kama kielelezo cha mwanamke shujaa wa Kiislamu katika *Utenzi wa Fatuma*. *Jarida la Kiswahili Sanifu, 3*(2), 1–9. https://doi.org/10.61889/h1g89q78

Kioko, K. M., Mavisi, R., & Nkumbo, D. (2025). Usawiri wa mwanamke wa kisasa katika filamu ya *Maria*. *Editon Consortium Journal of Kiswahili, 6*(1), 66–77. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.625

Mazrui, A. M. (2007). *Swahili beyond the boundaries: Literature, language and identity*. Ohio University Press.

Momanyi, C. (2012). *Usawiri wa mwanamke Muisilamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili* [Unpublished thesis]. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili: Chimbuko, kukua na kuenea kwake*. TUKI.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Noordin, M. M. (2006). Nadharia ya ufeministi wa Kiisilamu katika fasihi ya Kiswahili. In O. N. Oyori (Ed.), *Nadharia katika taaluma ya Kiswahili na lugha za Kiafrika*. Moi University Press.

Oso, W., & Onen, D. (2005). *Writing research proposal and report: A handbook for beginning researchers*. Jomo Kenyatta Foundation.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Press and Publishing Centre.

Taib, A. H. (2021). Mafundisho ya iktibasi katika *Utenzi wa Mtu ni Utu* wa Ahmad Nassir Juma Bhalo (Ustadh Bhalo). *Kioo cha Lugha, 9*(1), 128–144. https://journals.udsm.ac.tz/index.php/kcl/article/view/4788/4127